Al-Ikhwan Al-Muslimoon (The Muslim Brotherhood)

© Quran wa Sunnah Society of East Africa – E-books 2005. www.qssea.net

CHAMA CHA AL-IKHWAN AL-MUSLIMUN (THE MUSLIM BROTHERHOOD) KILIANZISHWA NCHINI MISRI (EGYPT) MNAMO MWAKA WA 1928 NA HASSAN AL-BANNA (1906-1949). HUYU ALIKUWA NI MWANA-HARAKATI ALIYEKUJA KU-HUISHA FIKRA ZA TARIKA ZA KI-SUFI. NA HILI NI KUNDI LILILOANZISHWA NA HASSAN AL-BANNA LENYE KUTOA HUDUMA ZAKE KAMA MWAVULI WA USHIRIKIANO ILI KUWARIDHISHA KILA MMOJA JUU YA KILA KITU, PASI NA KUJALI KUHUSU UPOTOFU KWENYE AQEEDAH NA MFUMO WA MANHAJ.

Baada ya uvamizi wa kijeshi wa Uingereza katika nchi ya Misri, ghadhabu za al-Banna kwa mabepari wa ki-magharibi zilizidi kutokana na ubakuraji wa uchumi wa nchi na kutawaliwa kiutamaduni. Ni kwa sababu hiyo, ndipo al-Banna akaona inafaa kuanzisha kipote cha ki-Islamu ambacho kitakachopinga mielekeo ya **"Usekula *(Secularism)"*** na uharibifu wa nchi na jamii nzima uliokuweko kwa kujitokeza na kudai haki ya kurudisha utamaduni wa ki-Islamu na njia zake za kimaisha. Alianza kupenyeza fikra za jumuiya hii ndani ya jamii ya wa-Misri kwa kutegemea mipango ya huduma za kijamaii zilizokuwepo tangu zamani. Kundi hilo liliwavutia, kwa jinsi ya mapatano, wengi miongoni mwa wana-harakati wapya na kuanzisha mabiashara chungu nzima, vituo vya kuwahudumia wagonjwa na mashule. Katika kutoa mwito katika vijiji mbali mbali, al-Banna akaanza ukaguzi wa wafuasi kutoka katika kila sehemu za jamii ya wa-Misri kwa kuwahutubia kuhusu mas-ala kama vile Ukoloni, huduma za afya, halmashauri ya kielimu, usimamizi wa mali za asili, U-maxi (Marxism), ubaguzi wa kijamii, Uzalendo wa Uarabu, udhaifu wa ulimwengu wa ki-Islamu na vita vinavyo pamba moto vya wa- Palestina.

Al-Banna hakuanzia wala hakumalizia mwito wake na misingi ya ‘aqeedah ya ki-Islamu, *at-Tawheed* (kumpwekesha Mwenyezi Mungu katika hali zote za ‘Ibaadah), kama ilivyokuwa njia ya Mitume. Al-Ikhwan al-Muslimun wameendelea kutojali msingi muhimu wa kuwalingania wafuasi wao kwenye mwito wa *Tauheed* na kuwakataza na mambo ya ushirikina, kwa sababu haya ni mambo yanayohitaji wakati na juhudi ili kuyabadilisha, mambo ambayo si rahisi kwa watu kuyakubali. Al-Ikhwan al-Muslimun walikuwa wakijishughulisha sana na kujumuisha wingi wa makundi ya watu badala ya kuwalingania watu kwenye njia ya Mtume (Mwenyezi Mungu amzidishie daraja yake na ampe amani).

Kwa sababu hiyo, wao wanamkaribisha kila aina ya wazushi katika mambo ya dini kwenye vyeo vyao, wakiwapa majukwaa walinganie waziwazi kwenye imani zao mbalimbali zenye kuhitilafiana. Miongoni mwa al-Ikhwan al-Muslimun wanapatikana wafuasi wa *Sufi*, *Jahmiyyah* (wale wenye kukanusha yakwamba Mwenyezi Mungu ana sifa zozote), *Shiaa’*, *Mu’tazilah* (madh-hab ya *‘ilm ul Kalaam* (philosophical) ambayo pia inakanusha sifa za Mwenyezi Mungu), *Khawaarij* (wale wenye kuwatoa watu nje ya mkunjo wa Uislamu kwa ajili ya utendaji wao wa madhambi), Waislamu-mamboleo (*modernists*), na wengine wengi. Matokea ya mfumo huu wa

© Quran wa Sunnah Society of East Africa – E-books 2005. www.qssea.net

kujifaidisha ki-siasa ni kuubadilisha ubainifu wa Uislamu na badala yake kuanzisha mambo ya uharibifu na upotofu. Amesema Mwenyezi Mungu:

Utawadhania kuwa wako pamoja, kumbe nyoyo zao ni mbali mbali. Hayo ni kwa kuwa wao ni watu wasio na akili. [Soorah al-Hashr 59:14]

Kundi hili lilipozidi kustawi kwenye miaka ya 1930, lilibadilika kwa kasi kubwa na kujiimarisha na kuanza harakati zenye kuhusika pasi na kizuizi kwenye ukumbi wa siasa za Misri. Katika kuhusika kwao na kuwashambulia viongozi, shirikisho hili likaanza siasa za chini kwa chini. Uzushi wa aina hii wa chini kwa chini katika Dini, sasa unaweza kuonekana katika mapote mengine yaliyo hatari zaidi kama vile *al-Qaa'edah* na *Jamaa'atul-Jihaad*. Baada ya mifululizo ya mauaji ya siri ya hapa na pale baina ya wanachama wake na serikali, Waziri Mkuu Nuqrashi Pasha alilipiga marufuku kundi hilo mnamo mwezi wa December 1948. Ijapokuwa (kundi lao) lilifuata njia za utulivu bila ya ghasia wala fujo katika ulinganizi wake tangu miaka ya sabiini (1970s), lakini wamewaandalia makundi mengine ya Qutubiyyah jukwaa ambalo litakaloendeleza harakati hizo kuanzia pale walipokoma wao.

Ni miongoni mwa misingi ya itikadi za al-Ikhwaan al-Muslimun ni kuamini yakwamba ardhi zote, kila chenye kumilikiwa, na damu za mataifa ya ki-Islamu kuwa ni haki zao, utadhani yakwamba mataifa hayo ni mahali pa majaribio. Kwa sababu hiyo, wao huangamiza vizazi kwa vizazi vya watu kwa min-ajil ya kujinyakulia utawala. Wao huamini yakwamba wana uwezo wa kufanya jitihada na utafiti wao wenyewe wa njia tafauti za kuuimarisha Uislamu, kama kwamba haya Maandiko ya Uislamu hayana muongozo wala njia za ki-Sheriya zilizowekwa kwa makusudio haya. Hapa waziwazi wameikhalifu njia ya mitume katika kuwalingania watu kwa Mwenyezi Mungu, ndio mpaka leo bado hawajapata chochote chenye kufanana na Ushindi.

HASSAN AL-BANNA:

Ni Sufi mkubwa na vilevile ni Mufawwidh (mwenye kuzikanusha sifa za Mwenyezi Mungu), kama alivyonukuu yeye mwenyewe yakwamba atafanya ziara kwenye makaburi na kujishughulisha na mambo mengi ya uzushi.

SAYYID QUTB:

Alikuwa na utaalamu mkubwa wa uandishi wa vitabu na wala hakuwa ni Mwanachuoni, Sayyid Qutb alifanya makosa mengi sana makubwa makubwa katika misingi ya 'Aqeedah na akazua rai nyingi ambazo zilizosababisha mazazi ya harakati za kisiasa zenye upotofu.

ABU A'LA MAUDUDI:

Huyu ni mtu aliyewatukana Mitume wengi wa Mwenyezi Mungu na maswahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وسلم na vilevile akachochea juu ya njia isiyokuwa ya ki-Islamu ya fikra za mapinduzi.